# Jinsi ya kumaliza umasikini wa kifamilia

MAOMBI ABEL CHAGAMBA

# YALIYOMO


**NENO KUTOKA KWA MWANDISHI** ........ 2

**UTANGULIZI** ........ 4

**SEHEMU YA KWANZA** ........ 7

2) KUNA KIZAZI KINACHOJENGA BARABARA, KUNA KIZAZI KINACHOENDELEZA BARABARA NA KUNA KIZAZI KINACHOPUMZIKA NA KUFAIDI MATUNDA YA VIZAZI VILIVYOPITA ........ 17

3) ELIMU YA SHULENI SIO UFUNGUO WA MAFANIKIO ........ 25

4) KITU AMBACHO HAKINA MAANA KWAKO KINAWEZA KUWA NA MAANA KUBWA KWA KIZAZI CHAKO KINACHOKUJA. ........ 28

**SEHEMU YA PILI** ........ 33

1) USIWE MVIVU WA KUFANYA KAZI ........ 33

2) TUMIA KIPAJI CHAKO ........ 39

FUATA HELA ILIPO AU LAZIMISHA HELA IKUFUATE ........ 47

1) FUATA HELA ILIPO ........ 47

1) ILAZIMISHE HELA IJE KWAKO ........ 49

JINSI YA KUHAMISHA URITHI KWA KIZAZI KINACHOFUATA........ 51

## FIKIRI VIZAZI VITATU KUTOKA KWAKO (THINK IN TERM OF 3 GENERATION FROM YOU)

*A good man leaves an inheritance to his children's children*

*Bible AKJV*

Ulishawahi kuwaza kama babu yako angekuwa anafanya mambo yake huku akiwaza ni jinsi gani utaishi hapa duniani maisha yako yangekuwaje?,ukitaka kumaliza umasikini katika familia yako na hapa namaanisha kuwa kama kuna siku wewe uliwahi kulala njaa basi mjukuu wako hiyo siku asiione, basi inabidi ufikiri vizazi vitatu vijavyo.

Na hapa ndio tunaanza kupotezana na Watanzania kwani fikra zao ni pua na mdomo huwa hawaoni madhara ya kile ambacho wanakifanya siku za mbele kwa watoto wao na wajukuu wao na ndio maana utakuta mtu anaingia mkataba ambao ni mbovu ili mradi apate pesa kidogo tu ya kula yeye leo bila kujali kuwa huo mkataba mbovu alioingia utakuja kuwatesa wajukuu zake, anachoangalia mimi nitapata nini leo na akiona kuna faida basi hajali nini kitatokea kwenye kizazi kinachokuja ila kama ukianza kufikiri kwa vizazi vyako vitatu basi hata jinsi unavyotumia pesa itakuwa tofauti na hata jinsi ambavyo unawekeza itakuwa tofauti.

Vitu huwa vinaokena tofauti ukiviangalia kwa jicho la muda mrefu, nikupe mfano mdogo miaka kadhaa iliyopita wakati niko chuo niliamua kuanza kuwekeza kwenye ardhi na maono yangu yalikuwa ya miaka 6 mbele, yaani ninacho maanisha ni kuwa nilikuwa nanunua ardhi leo ila mipango yangu ni kuitumia miaka 6 ijayo, kwa hiyo baada ya kutafuta ardhi nikapata sehemu

ambayo ilikuwa bado haijaendelea kabisa kwa jicho la mwaka ule ili ukiangalia kiwanja kile kwa jicho la miaka 6 kiwanja kile kina thamani kubwa mno, nikaongea na mwenye kiwanja akaniambia kuwa ataniuzia kwa laki tatu na ishirini, kiwanja kilikuwa kizuri ila kilikuwa maeneo ambayo hayajaendelea, kwa hiyo bei yake ilikuwa chini pia, baada ya kukinunua nikakaa kama miaka 4 lile eneo likawa limeendelea sana na viwanja vikaanza kuuzwa kwa mamilioni na sio laki tena na miaka 6 baada ya mimi kununua jirani ilimbidi kununua kwa milioni 15 kiwanja.

Kitu ambacho nataka uone ni kuwa kama ningekuwa sifikirii kwa muda wa miaka 6 mbeleni kile kiwanja ningekiacha ijapokuwa kilikuwa na bei ya chini, hivi unafahamu kuna vitu ambavyo unaweza kuvifanya leo ambavyo vitakugharimu pesa kidogo sana ila vitawafaa sana wanao na wajukuu zako kiasi kwamba wanaweza kuishi kifalme katika siku zao.

Nikupe mfano kuna ardhi ambayo unaweza kuinunua leo hii kwa gharama nafuu sana ambayo kwako wewe haina manufaa sana ila kwa kizazi cha wanao au wajukuu zako itakuwa ni moja kati ya vitu vya thamani ambavyo umewaachia, Moja kati ya sababu nchi za kiafrika unakuta umasikini hauondoki katika familia ni kuwa kila mtu ana kifikiri kizazi chake tu na baada ya hapo kizazi kinachofuata kinaanza upya tena yaani hakuna mali ambazo zinaweza kutembea kizazi kimoja mpaka cha tatu.

Jaribu kufikiria mtu aliyechukua silaha na kwenda vitani kwa ajiri ya kupigania uhuru akiwa na uelewa wa kwamba huenda akapoteza maisha na huo uhuru ambao anaupigania asiweze kuona ila akiwaza kuwa hata kama mimi sitaona uhuru ambao mimi ninaupigania ila kizazi changu kitakuwa huru na hii inampa moyo wa kupigania kitu ambacho wajukuu zake au vitukuu ndio watafaidika

embu fikiri kama wazee wetu wangewaza ya kuwa kizazi ambacho kitakuja kitajijua chenyewe na kila mtu apiganie cha kwake mwenyewe, leo hii tungekuwa na uhuru?
Kwa hiyo ukitaka kizazi chako kijacho kisione njaa na umasikini inabidi uanze kufikiri kwa niaba yao pia, ili siku zao zikifika wasianze kujenga tena kutokea mwanzo ila wawe na msingi ambao umewajengea nimeuliza hapo mwanzo chukulia kama babu yako angefanya mambo yake huku akikuwazia na wewe leo hii ungekuwa na maisha gani?

## Nikupe stori moja

Miaka kadhaa iliyopita kulikuwa na vijana wawili mapacha mkubwa alikuwa anaitwa Esau na mdogo alikuwa anaitwa Yakobo, huyu Esau alikuwa muwindaji na Yakobo alikuwa ni mchungaji, siku moja Esau wakati anatoka kuwinda alikuwa na njaa sana akamkuta mdogo wake amepika chakula akamwambia nipe chakula na Yakobo akamwambia sikupi chakula hiki bure bali tubadilishane na haki ya uzaliwa wa kwanza, Esau kwa kuwa alikuwa na njaa sana akaona sio kitu kikubwa akasema hakuna shida chukua uzaliwa wa kwanza na mimi nipe chakula na ikawa hivyo, sasa katika tamaduni zao ni kuwa mtoto wa kwanza ndio mrithi wa mali nyingi za nyumbani kwa hiyo Esau alipouza haki ya uzaliwa wa kwanza alikuwa amepoteza kila kitu ila yeye hakujali kwani fikra zake zilikuwa za muda ule ule na fikra za Yakobo zilikuwa za vizazi vijavyo, sasa hawa watoto wawili walikuwa ni watoto wa mtu mmoja anaitwa Isaka na huyu Isaka alikuwa mtoto wa Ibrahimu na Baraka ambazo MUNGU aliweka kwa Ibrahimu zilienda kwa Isaka na kisheria Baraka hizi zilitakiwa kwenda kwa Esau kwani ndio alikuwa mzaliwa wa kwanza lakini kwa kuwa hakujali hili akapoteza Baraka zote zikaenda kwa Yakobo na leo hii tunajua nchi ya Israeli ambayo imetengenezwa na

makabila kumi na mawili ambao walikuwa watoto wa Yakobo ila ya Esau hatuyajui na biblia inasema Esau alihuzunika na kujuta sana baadae baada ya kukosa zile Baraka ila kama angewaza kuwa kuuza kwake haki ya uzaliwa wa kwanza kungeathiri hata vizazi vijavyo asingeuza ile haki kwa mlo wa siku moja.

Hiyo stori sio enzi zile tu kuna nchi leo zinaingia mikataba ili zitape msaada wa siku moja tu bila kujua zinaweka vizazi vyao vijavyo kwenye utumwa kwa sababu ya njaa ya siku moja.

# FALSAFA YA KUSIMAMA JUU YA BEGA LA KIZAZI KILICHOPITA

Hebu fikiria kama kila kizazi ambacho kingekuwepo kabla yetu sisi kingekuwa kinawaza kutatua matatizo yao wenyewe tu au kufanya vitu ambavyo vina manufaa kwao tu maisha yetu yangekuwaje, nikufikirishe shule ambayo umesoma ni shule ambayo haikujengwa na wewe, kuna baadhi ya shule na vyuo vimejengwa na kizazi cha tatu kabla yetu na sisi tunapokuja tunafaidi matunda ya kazi ambayo ilifanywa na wazee chukulia kama kila kizazi kingetakiwa kujenga shule zao, barabara na hosipitali zao leo hii tungekuwa wapi?.
Kama kila kizazi kitakuwa kinaanza mwanzo na sio kuanzia pale ambapo kizazi kilichopita kilipoishia hatuwezi kumaliza umasikini, siku zote ukitaka kuona mbali zaidi ya unavyoweza kuona kwa kimo chako inabidi usimame kwenye bega la mtu ndipo unapoweza kuona mbali zaidi.

Kama ukitaka kuona umasikini katika familia yako unaondoka basi inabidi ujifunze kutoa bega lako ili kizazi kijacho kiweze kusimama katika bega lako na kuona mbali zaidi, ila kama unahisi sio majukumu yako basi hii ndio moja kati ya sababu hata wewe hauwezi kuona mbali zaidi kwani watu waliotangulia katika familia yako hawa kuliona hili na kutoa bega lao kwa ajili ya wewe kusimama  na kuona mbali zaidi yao.

# ULISHAWAHI KUWAZA URITHI GANI UTAAWACHIA KIZAZI KIJACHO.

Amini usiamini kuna siku moja utazeeka na kuondoka hapa duniani ulishawahi kuwaza ni urithi gani utawaachia kizazi kinachokuja baada yako au unapenda ukumbukwe tu kwa kuwaachia wanao jina la ukoo, huwa nakutana na vijana wengi ambao huwa hawana wazo kuwa siku moja watazeeka na kama wasipo jipanga jinsi gani watakabiliana na uzee na badala ya kuwa ndio muhimili wa watoto wao na wajukuu zao wao ndio wanakuwa wategemezi wa watoto wao na hivyo unakuta kila kizazi kinaanza mwanzo na umasikini hauondoki katika familia.

Turudi kwenye stori yetu hapo juu, yule mzee hata pesa ambayo alipata kwa ajili ya kujenga nyumba ya chumba kimoja ni pesa ambayo aliipata baada ya kuuza nyumba ya urithi, chukulia kama hakukuwa na nyumba ya urithi ya kuuza angekuwa wapi.

Hata wewe hapo ulipo kwa umri wowote ule ulionao inabidi uwe na mikakati ya nini unaaachia watoto na wajukuu zako na sio kuamini uongo ambao tunaambiwa kila siku kuwa urithi wa mtoto ni elimu hii ya darasani *(urithi wa mtoto ni elimu yenye manufaa na mali)*, kama ni hivyo kusingekuwa na hospitali na barabara ambazo zimeachwa na kizazi kilichopita kwa ajii ya manufaa yetu
Na hayo rafiki yangu ndio maendeleo kwani kizazi kinachokuja kinaanzia kizazi kilichopita kilipoishia na kuendeleza mikakati na shughuli zilizoanzishwa na wazee wao, kama nchi haziwezi kuendelea bila urithi kutoka kwa kizazi kilichopita haudhani kuwa ni muhimu zaidi kwa wewe binafsi kuwa na urithi

madhubuti kwa ajiri ya watoto wako na wajukuu zako, Au unataka wewe uitwe masikini, mtoto wako aitwe masikini na mjukuu wako aitwe masikini wakati ulikuwa na nafasi ya kubadilisha majina ya watoto wako na wajukuu zako.

## VITABU VINGINE VYA MWANDISHI

1) ***FALSAFA YA UWEKEZAJI (jinsi ya kufikiri kama muwekezaji)***
2) ***JINSI YA KUSOMA RIPOTI ZA FEDHA (jinsi ya kuongeza ufanisi katika mshahara na biashara)***
3) ***UTT AMIS KWA MTU MWENYE HARAKA (muongozo mwepesi wa kuwekeza UTT AMIS***
4) ***JINSI YA KUWEKEZA KATIKA SOKO LA HISA LA DSE***

JINSI YA KUPATA VITABU, WASILIANA NA MWANDISHI KWA MAWASILIANO HAPO CHINI

Written by bro chagamba

**©Maombi A. Chagamba**

**Simu: +, 0713999596**

**WhatsApp: +255713999596 au**

**Email wiseinvestorr@gmail.com**